



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

WAKALA WA MAJI NA USAFI WA
MAZINGIRA VIJIJINI



Barabara ya Mbesa, S. L. P 66Tunduru - Ruvuma, Tanzania
Simu: +255 25 2680016, Tovuti: www.ruwasa.go.tz, Barua pepe: tundurudm@ruwasa.go.tz

Tarehe 12/03/2024

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA UFUNDI BOMBA NA UHASIBU KWENYE
VYOMBO VYA WATOA HUDUMA YA MAJI NGAZI YA JAMII**

Meneja wa RUWASA Wiliya ya Tunduru kwa niaba ya vyombo vya watoa huduma ya maji ngazi ya jamii vilivyopo Wiliya ya Tunduru anapenda kuwatangazia watanzania wenye sifa kujaza nafasi za kazi zifuatazo.

1. MHASIBU WA CHOMBO - NAFASI (4)

SIFA ZA MUOMBAJI.

1. Awe raia wa Tanzania
2. Awe na Elimu kuanzia cheti cha Fundi Sanifu Daraja la III na kuendelea
3. Awe na umri kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45
4. Awe ni mtu mwaminifu na mwadilifu ambaye hajawahi kuhukumikiwa kwa makosa ya jinai
5. Awe na uwezo wa kufanya kazi bila kusimamiwa.
6. Awe na uwezo wa kutumia kompyuta hasa, Microsoft Word, Microsoft Excel, na Microsoft powerpoint.
7. Awe tayari kufanya kazi maeneo ya vijijini.

MAJUKUMU YA MHASIBU.

- I. Kuwa Msimamizi mkuu wa masuala yote ya kifedha katika Chombo Cha watoa huduma ya maji Kusimamia ukusanyaji wa malipo Ankara za maji kwenye vituo vyote vya kuchotea maji
- II. Kuandaa bajeti ya mwaka ya Chombo Cha watoa huduma ya maji
- III. Kuandaa taarifa zote za kifedha na kuziwasilisha kwa msimamizi wa Chombo Cha watoa huduma ya maji
- IV. Kufanya malipo baada ya kuidhinishwa na Msimamizi wa Chombo Cha watoa huduma ya maji na Meneja wa RUWASA Wilaya.
- V. Kutunza vitabu vya fedha, hati za malipo na Nyaraka zote za uthibitisho wa malipo na matumizi ya fedha za shughuli husika.
- VI. Kupeleka fedha zote benki za makusanyo ya Ankara za maji kabla ya matumizi.

- VII. Kushauriana na Msimamizi wa Chombo Cha watoa huduma ya maji katika masuala yanayohusu fedha katika kutekeleza shughuli zote za Mradi.
- VIII. Kutunza vitabu vya fedha, hati za malipo na nyaraka zote za uthibitisho wa malipo za matumizi ya fedha za shughuli husika
- IX. Kupeleka fedha zote za makusanyo ya Ankara za maji benki kabla ya matumizi
- X. Kushauriana na msimamizi wa chombo katika masuala yanayohusu fedha katika kutekeleza shughuli zote za mradi.

2. FUNDI BOMBA - NAFASI (9)

SIFA ZA MUOMBAJI .

- 8. Awe raia wa Tanzania
- 9. Awe na Elimu kuanzia cheti cha Fundi Sanifu Daraja la III na kuendelea
- 10. Awe na umri kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45
- 11. Awe ni mtu mwaminifu na mwadilifu ambaye hajawahi kuhukumiwa kwa makosa ya jinai
- 12. Awe na uwezo wa kufanya kazi bila kusimamiwa.
- 13. Awe na uwezo wa kutumia kompyuta hasa, Microsoft Word, Microsoft Excel, na Microsoft powerpoint.
- 14. Awe tayari kufanya kazi maeneo ya vijijini.

MAJUKUMU YA FUNDI.

- i. Kuwa Msimamizi mkuu wa CHOMBO ya watumiaji maji katika ngazi ya Jamii na Katibu wa Watumiaji maji.
- ii. Kusimamia, Kutafuta na kutekeleza shughuli zote za uendeshaji wa Mradi wa Maji.
- iii. Kusimamia ukusanyaji wa Ankara za maji na kutunza nyaraka zote za shughuli za uendeshaji wa Mradi.
- iv. Kusimamia utoaji wa Maji yenye ubora yanafika wateja/ wananchi;
- v. Kukusanya bili za maji;
- vi. Kusimamia Matengenezo ya Mradi na kutoa ushauri wa kiufundi kwa CHOMBO na Meneja wa RUWASA Wilaya.
- vii. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Mradi.
- viii. Kuhamasisha uchangiaji wa Huduma ya maji, kutatua na kusuluhisha migogoro baina ya Mteja/mwananchi na CHOMBO
- ix. Kuandaa taarifa za uendeshaji wa Mradi, Mfano Mapato na matumizi na kuziwasilisha kwa Meneja wa RUWASA na CHOMBO ya Watumiaji maji.

- x. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa Shughuli za Mradi za mwezi, robo na mwaka na kuziwasilisha kwa meneja RUWASA na CHOMBO ya Watumiaji maji.
- xi. Awe tayari kufanya kazi zingine atakazopangiwa na Viongozi wa CHOMBO na meneja wa RUWASA Wilaya
- xii. Kufanya Manunuzi ya Mahitaji ya Mradi kwa kufuata taratibu za manunuzi ya umma.


MASHARTI YA KAZI/ MSHAHARA

1. Kazi hii ni ya mkataba, mkataba unaweza kuhuishwa na mwajiri wa chombo cha watoa huduma ya maji ngazi ya jamii CBWSO kutokana na utendaji kazi mzuri wa mwajiriwa
2. Malipo kwa mwajiriwa yatatokana na makusanyo/mauzo ya maji ya chombo husika.

MAELEZO YA JUMLA.

Maombi haya yawasilishwe kupitia email adress ya ofisi ya Meneja wa RUWASA tunduru. tundurudm@ruwasa.go.tz . Mwisho wa kupokea maombi haya ni 26/03/2024.

Tangazo hili limetolewa na Meneja wa RUWASA Wilaya ya Tunduru kwa niaba ya vyombo vya watoa huduma ya maji ngazi ya jamii


.....

Eng. Maua J. Mgallah

MENEJA - RUWASA (W)

WILAYA YA TUNDURU

